

Sehemu ya kitabu

MTAZAMO WA WANAMKE WENGI LEO

Wanawake wengi wanaamini waliumbwa wawe kama wanaume, hivyo wanawake wengi wamekuwa wakiamini kwamba ili wapate haki zao ni lazima washindane na wanaume, hii imepelekea kuzaliwa mtazamo ambao unawaonyesha wanawake kuwa wakifanya kile wanaume wanafanya basi watakuwa sawa na wanaume.

Ni hakika kuwa hakuna mwanaume anayetaka kuwa na mwanamke anayetaka kushindana naye, isipokuwa mwanaume hutekwa na mwanamke mnyenyekevu pekee.

Mwanamke hauwi mwanamke kwa kutaka kushindana na mwanaume isipokuwa unakuwa mwanamke kwa kukubali wajibu wako na kukaa kwenye nafasi yako. Wanawake wengi waliofankiwa hasa katika ndoa zao ni wale waliokubali nafasi zao na kufanya wajibu wao kwa moyo wa kupenda.

Hakuna namna nyingine ya kumshawishi mwanaume akuchukulie kama mwanamke zaidi ya kukaa kwenye nafasi yako.

Mwanaume hatekwi kwa kumuonyesha unaweza zaidi yake, mwanaume anatekwa kwa unyenyekevu na utii.

Mwanamke ukijua wajibu wako na kufanya majukumu yako kumteka mwanaume ni kazi nyepesi sana.

UDHAIFU AMBAO NI NGUVU YA MWANAMKE

Mwanamke ni funguo muhimu kwa mafanikio ya mwanaume na wanaume werevu pekee ndio hilitambua hili. Hivyo huwatunza kwa namna ya upekee na uangalifu wa viwango vya juu.

Mfano mzuri kwa wanandoa katika 1 petro 3:7 anasema ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu; na kama warithi pamoja na neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe.

Mungu ameambatanisha majibu ya maombi ya mume pamoja na mahusiano ya kifikra na mke wake.

Hii inaonyesha jinsi mwanamke alivyo na umuhimu machoni pa Mungu. Mwanaume asitegemee kuharibu kwa mke wake na kutegemea Mungu atajibu maombi yake.

Mtume Petro anapoongelea udhaifu hapa hana maana kwamba hawana nguvu ila anamaana kwamba mwanamke anakuwa kwako kutokana na vile unavyomchukulia na kumtunza.

Neno udhaifu hapa halionyeshi au halisimamii kwamba wanawake kuna kitu wamepungukiwa, ila lilitaka kumtambulisha mwanaume aliyepewa mamlaka kwanza atambue namna ya kumtunza mwanamke.

Naweza kusema Mungu amekupa mtu wa kukusaidia sawa, lakini mtu huyo atakusaidia kulingana na vile utakavyomruhusu akusaidie. Hivyo mtazamo bora wa

mwanaume juu ya mwanamke kutokana na mstari huo ndio utakao amua mwanamke awe wa namna gani kwake.

Sio kwamba mwanamke hana uwezo wa kukusaidia hapana! Ila uwezo wake unategemea sana mwanaume unajua nini kuhusu huo uwezo wake.

Hata kama mwanamke ana uwezo zaidi ya aina hamsini lakini wewe ukafahamu aina mbili tu za uwezo wake basi ndizo utakazo zitumia hizo hata kama zingine zipo.

Na ukeli ni huu hata kama hujui uwezo wake mwingine haikufanyi umuone mwanamke ni chombo kisicho faa ila ni ufahamu wako ndio wenye shida. Kwa mfano kama hujui kuitumia kompyuta tatizo sio la kompyuta ila ni lako mtumiaji, ndivyo ilivyo hata kwa mwanaume asiyejua uwezo wa mwanamke.

Ndio maana ya udhaifu uliyotajwa na Mtume Petro katika mstari huo. Mwanamke hawezi kuinuka akafanya mwenyewe kwasababu amewekwa afanye kazi chini ya mamlaka ya mumewe, hivyo wakati wote anasubili neno la mumewe na ndilo humpa nguvu.

Mwanamke ameumbwa kupokea hivyo wakati wote atatafuta mwelekeo kutoka kwa mumewe na mwelekeo huo ndio utaamua atumie vipi nguvu zilizo ndani yake.

Hii ndo sababu tena mtume Petro aliandika tuishi nao kwa akili, ni kwamba inawahitaji wanaume wawe na uwezo fulani wa maarifa ili kuweza kuishi nao na kutumia uwezo ulio ndani yao kwa manufaa na kujenga.

Hivyo mwanamke sio mdhaifu kama wengi walivyozoea kusema, ila ni chombo kilichobeba nguvu nyingi na

kinahitaji mtu wa kukielekeza mahali pa kuitumia nguvu hiyo. Wakati mwingi mbele anaonekana mwanaume lakini nyuma yake yupo mtu anayefanya kazi ya kumsababisha mwanaume aonekane naye si mwingine ni mwanamke.

Huwenda ningesema katika sekta nyingi ambazo tunaona wanaume wanaongoza huwenda tumeongozwa na wanawake kwa sehemu kubwa pasipo sisi kujua. Kwasababu haimuhitaji nafasi ya kuonekana na watu ili mwanamke aongoze, yeye huongoza kwa hamasa anayotoa kwa mumewe.